**JAMHURJ YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLIJ IA**

**CHUO CHA UALIMU KATOKE**

Anuani ya simu,
Simu: : Mkuu wa chuo 0763815205
Makamu wa Mkuu wa chuo 0755239857
Mwadili wa wanachuo 0784607654
0757530588
Msajili wa wanachuo 0768154565/
0786885446
Barua pepe: katoketc.moe.go.tz / katoket@gmail .com. Nukshi:.........
Kumb.Na: CCU/KAT/JOIN/136

S.L.P. 1178 ,
**BUKOBA.**
16/05/2022

Bwana/Bibi/Bi....................................

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI/AWALI 2022/2023

I. **UTANGULIZI:** Tunayo furaha kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi(kama umechaguliwa kusoma Ualimu Elimu ya Msingi) na Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali(kama umechaguliwa kusoma Ualimu Elimu ya Awali) katika Chuo cha Ualimu Katoke.

**MAHALI CHUO KILIPO:** Chuo cha Ualimu Katoke kipo Mkoani Kagera, Wilaya ya Muleba. umbali wa Km: 50 kutoka Bukoba Mjini, ukifuata barabara iendayo Biharamulo; vilevile Km: 23 kutoka Muleba ukifuata barabara ya Biharamulo kuelekea Bukoba Mjini. Ukitokea Mwanza au Biharamulo kwa barabara, utafika kwanza Muleba kisha Katoke. Barabara hii hupitia katika eneo la chuo kiasi cha meta 300 kutoka kwenye majengo ya Chuo. Kama ni mchana, ni rahisi kupambanua kwani kibao kilichoandikwa **' Chuo Cha Ualimu Katoke'**, kipo barabarani. Ukifika unaongozwa na barabara yenye miti mirefu pande zote. **Ni karibu, usidanganywe na waendesha pikipiki.**

**DIRA YA CHUO:** Kuwa na Mwalimu Mweledi, anayemudu Mazingira, mwenye Fikra za Kiutandawazi na Nidhamu, anayekuza Utamaduni wa Taifa kwa Mtoto.

**MOTO YA CHUO:** "Nakaza Mwendo"

## 2. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

**A. VYETI NA VITAMBULISHO:** Ili kuthibitisha kuwa wewe ndiye uliyechaguliwa kujiunga na chuo hiki, LAZIMA uje na vitu vifuatavyo:-

(i.)Cheti halisi cha matokeo ya Mtihani/Mitihani (National form iv Certificate) au Result Slip halisi kwa wale waliohitimu Mwaka 2021

(ii.)Cheti cha shule kinachoonesha kuhitimu katika shule husika (school leaving certificate)/chenye picha/ saini na mhuri wa mkuu wa shule uliogongwa kwenye picha ya mhitimu na saini ya mkuu wa shule.

(iii)Cheti cha mganga anayetambuliwa na serikali kuthibitisha afya yako. Fomu

hiyo imeambatishwa. **KIAMBATISHO NA. 1**
(iv) Barua ya Chuo inayokuita kujiunga na chuo hiki.(Joining Instruction|(v)Cheti halisi cha kuzaliwa.
NB: **Vyote bapo juu ni muhimu sana kuja navyo chuoni.**

**B. ADA:** Kila mwanachuo atatakiwa kulipa **ADA Tsh. 450,000/=** (mia nne hamsini elfu) kwa mwaka, kwa ajili ya kugharimia mafunzo.Unaweza kulipa **Tsh. 225,000/=** (Mia mbili ishirini na tano Elfu) mwanzoni mwa kila muhula. Unasisitizwa kukulipa ADA inayotakiwa.

Fedha ya ADA hulipwa kwa kutumia namba ya utambulisho ya mlipaji (Control number) . Tafadhali wasiliana na mhasibu wa chuo kwa simu **namba 0745605563** ili akupatie control number utakayotumia kulipa ada tu.
NB.Kila mwanachuo aliyechaguliwa anatakiwa kuja na stakabadhi ya malipo ya ada . Jitahidi kulipia benki kwa control number uliyopewa na mhasibu.

**C 1. MICHANGO:** Michango mingine ambayo hutolewa chuoni huwekwa kwenye akaunti ya chuo, Benki ya **NMB- KATOKE TEACHERS' COLLEGE DEVELOPMENT FUND - ACCOUNT NO: 3200 110 00 03. Jitahidi kulipia benki kwa akaunti Uliyopewa hapo juu**


| Aina ya Mchango | Kiasi katika shilingi za Tanzania na muda |
|---|---|
| Usajili na kitambulisho | 20,000/= kwa mwaka wa kwanza tu. |
| Kukodi godoro | 10,000/= kwa mwaka |
| Ulinzi | 30,000/= kw a mwaka |
| Usafi na mazingira | 20,000/= kwa mwaka |
| Michezo | 30,000/= kwa mwaka |
| Serikali ya wanachuo | 5,000/= kwa mwaka |
| Huduma ya kwanz.a | 10,000/=kwa mwaka |
| Ukarabati | 25,000/= kwa mwaka |
| Bima ya Afya (NHIF) | 50400/= kwa mwaka |

**C 2. KADI YA NHIF: Kama huna kadi ya NHIF unatakiwa kuja na pesa taslimu Tsh. 50,400/= kwa ajili ya kulipia bima ya afya (NHIF) kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo juu. NI LAZIMA KULIPA BIMA YA AFYA KWA YULE AMBAYE HANA KADI YA BIMA YA AFYA.**


**D. SARE: WAVULANA** (i.) Suruali **Nyeusi** Mbili zisizobana na mifuko mitatu, miwili mbele na mmoja nyuma kulia ,upana wa suruali miguuni iwe ni **inchi 17** na urefu wake uweze kufunika soksi za viatu. (Angalia Picha ya suruali kama ilivyooneshwa katika picha namba 2 hapo chini) (ii.) Shati Mbili za Mikono Mirefu za Rangi ya Light Blue. (iii.) Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunika; Soksi jozi mbili nyeupe (iv.) Tai mbili nyeusi ndefu za kadri. (v.) Nywele ziwe zimenyolewa fupi.Haturuhusu vipara (vi)Nguo za ndani zakutosha.

**WASICHANA:(i)** sketi mbili **nyeusi** linda box, urefu wake ni **chini ya magoti** kuanzia sentimita 20, isiyobana popote katika maumbile ya mwili(angalia picha ya sketi ya wasichana katika picha namba 1 hapo chini). (ii) shati mbili za mikono mirefu za rangi ya light blue. (iii)bow-tai nyeusi mbili. (iv) viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vya kufunika miguu kabisa na visiwe na kisigino kirefu. (v) soksi nyeupe jozi mbili. Siku zote za kuwa darasani, nywele zitakuwa zimesukwa kawaida kuelekea nyuma au zimenyolewa ni fupi na nadhifu. Kwa wasichana waislamu, wataruhusiwa kuvaa hijabu ya rangi ya light blue kama unifonn ya darasani (isitofautiane na rangi ya shati)(vi)nguo za ndani pamoja na taulo)za kike (pedi) za kutosha.

**PICHA 1 (SKETI –WASICHANA)**



**PICHA 2 (SURUALI-WAULANA) si lazima iwe na pindo la miguuni kama mchoro unayoonesha**



**3. MAVAZI MENGINE MUHIMU**

**MICHEZO:** - (i.) Uje na bukta mbili za rangi ya blue na tisheti nyekundu mbili zenye kola,zisizo na maandishi yoyote wala rangi nyingine. (ii.) Uje na raba za michezo jozi mbili, na stockings Jozi mbili, moja bluu na nyingine kijani. (iii.) Track suit (blue), nayo ni kwa ajili ya michezo.

Katoke mara nyingi kuna mvua nyingi na baridi, hivyo ni vyema kuja na koti jeusi linalofanana na suruali AU Sketi ( Makoti au Jaketi za aina nyingine yoyote haziruhusiwi chuoni.) Uje na mwavuli, pamoja na viatu vya mvua (Rain boots).

**MAVAZI BINAFSI:-** Uje na nguo chache ambazo si sare ya chuo zenye hadhi ya kiualimu, ambazo utavaa ukiwa chuoni muda ambao hautakuwa wa darasani .Aidha nguo hizo zitatumika pia katika shughuli za kuabudu kulingana na Imani yako.

**4. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI:**

(i.) Gharama ya kukodisha godoro ni Tshs. I0,000 /= kwa mwaka kama inavyooneshwa katika jedwali la michango kwa watakaowahi,au waweza kuja na godoro lako lenye vipimo inchi2.5xfuti 6 kwa kuwa magodoro yaliyopo chuoni ni machache.

(ii.) Uje na shuka mbili (2) za rangi ya pink, blanke ti, mto na foronya za pink.

**5. MAIDTAJI MUHIMU KWA AJILI YA TAALUMA:**

Uje na madaftari ya kutosha yasiyopungua 14 makubwa, mathematical set, kalamu na penseli za
kutosha na rim 1 ya karatasi A4

**6. AFYA YA MWANACHUO:** Mwanachuo aliyechaguliwa atatakiwa kupimwa kuthibitisha afya yake. FOMU kwa ajili ya kupima afya imeonyeshwa katika **KIAMBATISHO NA. 1.** Matibabu hutolewa kwa magonjwa kama taratibu za NHfF zinavyoelekzea. Uwapo chuoni utapewa sehemu ya kulala, kitanda na chakula, lakini chuo hakitoi chakula maalum ( " special diet" wala " light diet"). Uje na sahani moja, bakuli moja, kikombe kimoja visivyokuwa vya plastic, na kijiko kimoja kwa ajili ya chakula. Unatakiwa uje na ndoo ya lita 20 kwa ajili ya usafi.

**7. MAIDTAJI BINAFSI YA MWANACHUO:** Utakuwa na uhuru wa kuabudu kwa dini na dhehebu lako. Wapo walezi washauri kwa kila dhehebu. Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na fedha za matumizi binafsi kwa ajili ya mahitaji yake madogomadogo awapo chuoni.

**8. TARATIBU ZA CHUO:** Ufikapo chuoni, Mwadili wa Wanachuo atakupa maelekezo ya namna ya kuishi chuoni. Utapewa nakala inayoonesha Kanuni na taratibu za chuo na fomu ya kujaza kukiri kufuata taratibu zote uwapo chuoni. Kwa kifupi utatakiwa uwe **"MWAMINIFU, MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU"** muda wote utakaokuwa hapa chuoni. Unakuja kujifunza ili uwe mwalimu bora unatakiwa kuweka juhudi katika masomo. Ukwepaji wa vipindi hauruhusiwi, utalazimika kuzingatia ratiba ya chuo.

MWISHO:Tunakukaribisha sana Chuo cha Ualimu Katoke, kwa matumaini kuwa utakuwa mwanachuo mwema, hodari, unayejiheshimu na kuwaheshimu wengine kwa mwenendo wako jumuiya nzima ya chuo ifurahie kuwepo kwako hapa chuoni. Chuo kitafunguliwa 13/06/2022, Hivyo unashauriwa kuwahi.

Tunakutakia Safari Njema.

**KARIBU SANACHUO CHA UALIMU KATOKE**

Michael F. Ntwale
MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO CHA UALIMU KATOKE
S.L.P. 1178 BUKOBA
KAGERA

KIAMBATISBO NA. 1

## GOVERNMENT OF TANZANIA
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

TO: The Medical Officer

From: ............................ .
Teachers' college

.............................................

......................................... ..

Please examine the above named as to his/her physica l and mental fitness for a full timeteachers course.

A: I. (a) Eye - sight
(b) ) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(t) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date: ........................

Signature ......................................

Official Stamp

.........................................................................

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally •fit/unfit for a full time teacher Education course.

(a) Eye - sight..............................................................
(b) Hearing...................................................................
(c) Limbs......................................................................
(d) Speech....................................................................
(e) Leprosy...................................................................
II. Neuroses....................................................................
III. Other serious diseases..................................................
IV. Pregnancy...................................................................

**Date:............ Signature.................................**

**Official Stamp**